

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
JESHI LA POLISI TANZANIA**



TANGAZO LA AJIRA

Jeshi la Polisi Tanzania linatangaza nafasi za ajira kwa vijana wenye fani mbalimbali ambazo zimeainishwa katika kiambatanisho namba 1 kilichoambatanishwa na tangazo hili.

Muombaji atatakiwa kuandika barua ya maombi kwa mkono wake mwenyewe (handwriting) kwa Inspekta Jenerali wa Polisi S.L.P 961 Dodoma.

Barua hiyo iambatanishwe na nakala ya cheti cha taaluma (Academic certificate), cheti cha fani aliyosomea, cheti cha kuzaliwa, cheti cha kumaliza shule (Leaving certificate), kitambulisho cha Taifa (NIDA) au namba ya NIDA.

Mwombaji anatakiwa kujaza fomu (kiambatanisho no 2) inayoonyesha taarifa zake binafsi, ambayo inapatikana kwenye tovuti ya Polisi. Utumaji wa fomu hiyo usiwe kwa njia ya kuskani (Scan) isipokua barua na vyeti vilivyotajwa hapo juu.

Maombi yote yatumwe kupitia barua pepe admin.phq@tpf.go.tz na sio kwa njia ya posta. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 29/9/2021.

Imetolewa na;
Inspekta Jenerali wa Polisi
Makao Makuu ya Jeshi la Polisi
S.L.P 961
DODOMA
21/09/2021